SHUJAA WETU..

NA

Aneth Mirambo

Amina alilia kwa uchungu, dunia ilionekana kumwangukia. Mazishi ya shangazi yake yalifanyika kijijini kwao.Baada ya msiba maisha yao yaliendelea kuwa mabaya kila kukicha. Wadogo zake wawili, Makoi wa darasa la sita na Kikoti wa kidato cha pili walilazimika kuacha shule na kuanza kazi ya bodaboda ili kujikimu.

Siku zilizidi kwenda na ilipopita arobaini baada ya msiba mwenyekiti wa serikali za mtaa, Mzee Mlilo, alifika nyumbani kwa kina Amina na kumpa matumaini mapya yeye pamoja na wadogo zake.

Amina, mimi na wazazi wengine wa kijiji tumekubaliana kupitia mfuko wetu wa kusaidia watoto wenye ufaulu mzuri, tutakusaidia uweze kuendelea na masoma, "alisema mwenyekiti kwa sauti ya upole lakini yenye matumaini". Amina alifurahi lakini hakuwa na uhakika wa kuwaangalia wadogo zake na kuweka kipaumbele kwenye masomo.

Kwa msaada wa serikali ya mtaa na wazazi wa kijiji chake aliweza kuendelea na masomo mpaka kufikia kidato cha sita akiwa na ufaulu mzuri sana wa alama 'A' na wakati huo wadogozake walikua wameshakomaa kwenye biashara ya Bodaboda.

Matokeo ya kupangiwa vyuo yalitangazwa na Amina alichaguliwa kusoma chuo kikuu cha ndoto zake shahada ya awali ya Uongozi na utawala bora. Alipofika Chuo hali ya maisha ilimkaba koo. Baada ya mwaka mmoja, alilazimika kusitisha masomo kwa muda kutokana na changamoto za kujikimu, Hivyo ilimlazimu Amina kurudi tena kijijini na kusaidiana na wadogo zake kwenye biashara ya Bobaboda ili kupata fedha za kujikimu.

Amina hakukata tamaa. Mwaka uliofuata alirudi chuoni, na safari yake ilichukua mkondo mpya kwani alijiingiza rasmi katika siasa.

Alianza kama kada mdogo wa chama cha Umoja wa Wananchi, lakini juhudi zake zilimfikisha mbali na kupitia uchaguzi wa Chuo Amina, alipata nafasi ya kuwa Makamu wa Rais katika chuo cha Millenium University.

Wakati huo Amina Allikuwa Akirudi likizo anawasaidia wadogo zake kwenye kilimo cha matikiti maji na taratibu sana maisha yao yakaanza kuwa na afueni. Jioni Amina na Wadogo zake walikuwa kwenye shambalao wakipalilia na kuzungumza.

"Dada, tunaweza kweli kufanikisha kilimo hiki?" Kikoti aliuliza akiwa anapanga miche ya matikiti.

"Ndiyo, Amina alijibu, hakuna lisilowezekana. Mnapaswa kuwa na nidhamu na kufanya kazi kwa bidii. Naamini maisha yetu yatabadilika na kuwa bora zaidi," Amina alihimiza na Makoi alitikisa kichwa ishara ya kukubali wosia wa dada yake.

Kikoti, ambaye alikuwa na shauku ya kujifunza zaidi, alimtazama dada yake kwa upendo. "dada, tutakupa sababu ya kujivunia. Tutafanya kazi kwa bidii hadi tuwe na shamba kubwa la mfano hapa kijijini," alisema kwa kujiamini.

Baada ya Miaka minne Amina alimaliza shahada yake ya kwanza na kurudi kijijini kwaajili ya kuendelea na shughuli mbalimbali za kimaeneleo na wakati huo alikuwa amechaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya vijana na wanawake.

Siku ya Jumatatu asubuhi majira ya saa mbili asubuhi, Jua lilichomoza taratibu katika kijiji cha Mbozi, mwanga wake ukigusa nyumba za udongo zilizojengwa kwa ustadi wa jadi.

Soko la kijiji lilianza kujaa watu, wakibeba bidhaa zao za kuuza. akiwa amevalia kitenge chenye rangi angavu,Amina na kamati yake walikuwa kwenye ziara ya Maendeleo ya kijiji. akizungumza na baadhi ya wanawake waliokuwa wakihangaika na changamoto za biashara zao.

"Mh Kiongozi, tunapambana lakini bado hatupati faida ya kutosha," alizungumza Mama mmoja mzee huku akifuta jasho usoni. "Kodi ya vibanda ni kubwa na wateja hawana pesa za kununua kama zamani."

Amina alitabasamu kwa upole, akishika mkono wa yule Mama Mzee kwa heshima. "Tutaangalia namna ya kuunda vikundi vya ushirika ili muweze kupata mikopo nafuu na kuendesha biashara zenu bila matatizo makubwa. Tunahitaji kuhakikisha kuwa wanawake wa kijiji chetu wanakuwa na uhuru wa kifedha."

Wananchi waliokuwa pale sokoni walishangilia kwa furaha, wakihisi kuwa hatimaye sauti yao ilisikiwa.

Ziara ikiwa inaendelea, Amina alikutana na vijana wa kijiji waliokuwa wakilalamika kuhusu ukosefu wa ajira. Mmoja wao, alisimama na kusema, "Mh Kiongozi, sisi vijana hatuna ajira, tunapoteza muda tu mitaani. Hatujui la kufanya."

Amina aliwaangalia kwa makini, akajibu kwa sauti yenye matumaini, "Tunahitaji kubadilika. Vijana tunapaswa kuwa na uwezo wa kujiajiri. Nina mpango wa kuanzisha mradi wa kilimo cha kisasa na ufugaji ili vijana waweze kushiriki na kujipatia kipato,

Wengine wakatikisa vichwa kwa kukubaliana naye. "Lakini tutapataje ardhi ya kulima na mtaji wa kuanzia?" aliuliza kijana mwingine.

Amina alitabasamu. "Tutashirikiana na wazee wa kijiji na serikali za mitaa kupata ardhi. Pia, nitahakikisha tunapata wawekezaji watakaotusaidia kuanzisha mradi huu. Lakini muhimu zaidi, tunahitaji kuwa na nia ya dhati na kujituma.

"Pia Serikali yetu kwa sasa inahamasisha vijana na wahitimu wa ngazi mbalimbali za taaluma kujiunga na VETA ili kuongeza ujuzi na maarifa kupitia fani ili kuliondoa taifa na wasomi wasio na ajira kwenye umaskini.

Hili lilikuwa jambo jipya kwa vijana Kwa mara ya kwanza, walihisi kuwa kuna mtu aliyewajali na kufikiria kuhusu mustakabali wao.

Katika baraza la wazee wa kijiji, Amina aliweka wazi dhamira yake ya kuboresha maendeleo. "Ndugu wazee, mnatufundisha mila na desturi, lakini pia tunahitaji maendeleo. Mimi ni mtoto wa kijiji hiki, nimekulia hapa, na nimeona changamoto zetu. Tukishirikiana, tunaweza kujenga shule mpya kwa watoto wetu na kuhakikisha kuwa huduma za afya zinaboreshwa."

Kiongozi mmoja Mzee wa makamo, alimsogelea Amina na kumwangalia kwa makini. "Umejaa maono, mwanangu. Haya si maneno ya kawaida. Ikiwa kweli umedhamiria, basi tuko tayari kuwa nyuma yako."

Kusikia hayo, Amina alijua kuwa alikuwa kwenye njia sahihi, yeye pamoja na kamati yake walianza kuandaa mipango madhubuti ya maendeleo, akifanya mikutano na wananchi, kusikiliza shida zao na kutoa suluhisho. Alianzisha mfuko wa kusaidia wanawake wajasiriamali, alihamasisha vijana kuingia katika sekta ya kilimo, na alianza kuzungumza na wadau wa maendeleo kuhusu kujenga shule na kituo cha afya kijijini kwao.

Mafanikio yake haya yalianza kumfanya ajulikane zaidi, na watu wengi waliona mwamko mpya wa matumaini kwa kijiji chao. Hapo ndipo alipoanza kutambua kuwa safari yake ya siasa haikuwa tu ya ndoto, bali ni wito aliopaswa kuutimiza kwa bidii.

Siku zilivyozidi kwenda Amina, aliteuliwa katika nyanja mbalimbali za Uongozi na alianza kuingia kwenye orodha ya viongozi vijana wenye ushawishi kwa kusaidia jamii yake, alijitoa kwa hali na mali kuhakikisha anafanya kazi zenye matokeo chanya. Baada ya kutambulika vyema kwenye siasa Wananchi walimpendekeza na kumtaka agombee ubunge kuwawakilisha wananchi wake, hivyo Amina aligombea Ubunge.

Lakini siasa haikuwa rahisi, kama mwanamke, alikumbana na changamoto nyingi. Wanasiasa wenye nguvu kama Mbunge Malongo walijaribu kumkwamisha kwa kumsababishia tuhuma nyingi za uongo, wengine walimtishia kwa sababu ya ushawishi wake aliokuwa nao. Wakati wa kampeni za ubunge wapinzani wake walihisi kuwa nguvu yake ni tishio kwao.

Katika mkutano wa siri, Malongo alikutana na wafuasi wake wa karibu, akiwemo Bw. Kandaya na Bw. Majuto.

"Huyu Mwanamke amekuwa tishio kubwa," Malongo alisema kwa hasira. "Ikiwa tutamruhusu aendelee, tutapoteza kila kitu. Tunapaswa kutumia kila mbinu kuhakikisha tumamzima kwa namna yoyoye ili niweze kuongoza hili jimbo."Hatuna tena muda wa kupoteza kipindi hiki cha Uchaguzi.

Kandaya aliguna na kusema, "Tunaweza kutumia vijana wetu wa kazi kazi, kumzuia kufanya kampeni. Pia, pesa zikizunguka, baadhi ya wazee wa kijiji wataungana nasi."Majuto naye alikazia, "Na tusisahau hofu! Tukizusha uvumi kwamba huyu Mwanamke anashirikiana na wageni kuharibu mila zetu, watu wataanza kumuogopa."

Njama zao zilianza kufanikishwa. Watu waliovaa kofia za giza walianza kufwatilia nyendo za Amina kila hatua. Akiwa kwenye gari na viongozi wenzake.Walimpita kwa kasi na ghafla tairi ya gari lake lilipigwa na kitu chenye ncha kali likapasuka. Gari lilipinduka mara tatu na kuanguka mtaroni.

Amina alihisi maumivu makali, damu ikitiririka kutoka kwenye paji la uso wake. Alijaribu kuinua mkono lakini hakuweza. Muda mfupi baadaye, alisikia watu wakikimbilia eneo la ajali, milio ya ving'ora vya polisi na ambulensi ikisikika kwa mbali. Alipelekwa hospitali na kulazwa kwa wiki mbili.

Wakati kampeni za uchaguzi zikiendelea kwa muda wa wikitatu Amina hakuweza kushiliki shughuli zozote za kampeni kwaajili ya kupigania uhai wake. Mungu si Athumani akiwa na majeraha mengi mwilini yaliyoanza kupata nafuu Amina alijilazimisha tena kusimama imara akapewa ulinzi wa kimila na mababu zake wa asili na Mungu, kisha alirejea tena kwenye kampeni za uchaguzi kwenye Jimbo lake akiwa na nia ya kuboresha miundombinu, na kuleta mabadiliko makubwa ya kimapinduzi. Uchaguzi ulihitimishwa na alishinda kwa kura nyingi na kuwa mbunge wa Jimbo Lake. Hakuwa mbunge wa maneno tu, alitimiza ahadi zake.

Katika kikao cha baraza la kijiji, Halima aliitisha mkutano mkubwa. "Ndugu zangu, tuliahidi maendeleo, na maendeleo hayaendi kwa maneno matupu. Tumepanga kujenga shule ya sekondari hapa kijijini ili watoto wetu wasiteseke kama tulivyoteseka sisi wakati tunatafuta elimu. Pia, tutajenga kituo cha afya ili akina mama wajawazito wasilazimike kusafiri umbali mrefu kwa matibabu wakati wa kujifungua."

Wananchi walimshangilia. Mzee mmoja alisimama na kusema, "Hakika wewe ni mfano wa kuigwa. Umetoka mbali, na sasa unatuongoza kwa maono makubwa. Tuko nyuma yako!"

Amina, aliweza kujenga shule ya Sekondari Tumaini kwa ajili ya watoto wenye mazingira magumu. Alianzisha mfuko wa kusaidia mabinti waliokuwa wakihangaika na changamoto za mahitaji ya shule, akiwapa msaada wa taulo za kike na vifaa vya masomo.

Wadogozake Makoi na Kikoti Waliweza kupanua kilimo chao na kuwaajiri vijana wengine wa kijiji katika mashamba yao makubwa ya Matikiti, Miti ya Mbao. Kikoti na Makoi walipata nafasi ya kwenda Veta kuboresha stadi zao za kilimo na baada ya muda Walianza ufugaji wa kisasa kwa kupata mbegu bora za Ngombe wa kisasa Sungura, Mbuzi mbuzi kuku na kondoo Kutoka South Afrika, pia walitafuta masoko ndani na nnje ya nchi jambo lililowaletea mafanikio na ubora wa shughuli zao za kilimo na Ufugaji.

Kwa muda wa miaka mitatu sasa Amina akiwa madarakani aliweza kutambulika kama Mwanamke mwanamapinduzi wa kimaendeleo anayesaidia jamii za watu wenye uhitaji wananchi wa Jimbo lake walimpenda na walifurahia uongozi wake.

MWISHO.